

## **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

### **HALMASHAURI YA WILYA YA MVOMERO**



**MVDC/L.10/1VOL.I/6**

**12/08/2021**

#### **TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kupitia kibali cha ajira mbadala chenye Kumb.Na. FA.170/361/01 "A"/144 cha tarehe 19/07/2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenyе sifa na ujuzi wa kujaza nafasi ifuatayo;

#### **1. Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (Nafasi 3)**

##### **a) Sifa za Mwombaji**

- Awe amehitimu Kidato cha Nne au Sita na Cheti cha Mafunzo (NTA LEVEL 5) katika fani mojawapo kati ya hizi; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology), Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

##### **b) Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III**

Mtendaji wa Kijiji atatekeleza majukumu yafuatayo;

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao
- Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo Kijijini
- Katibu wa Mkutano Mkuu na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika ngazi ya Kijiji.

### c) Ngazi ya Mshahara

Mwombaji atakayefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi

### 2. MASHARTI YA JUMLA

- i. Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti nya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) vilivyothibitishwa na wakili au Mahakama.
- ii. Mwombaji aambatishe picha mbili za rangi (passport size) za hivi karibuni
- iii. Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kwamba vyeti vyao vimehakikiwa na kuthibitishwa na mamlaka (TCU au NECTA) kulingana na ngazi ya Cheti
- iv. Maombi yaambatanishwe na maelezo binafsi (CV)
- v. Mwombaji awe na umri wa miaka 18 hadi 45

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero,

S.L.P 663,

### **MOROGORO.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06/09/2021 saa 9.00 alasiri.

**NB:** Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri  
[www.mvomerodc.go.tz](http://www.mvomerodc.go.tz)

Limetolewa na;



Hassani N. Hassani,

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
MVOMERO.**